THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/2

# KISWAHILI 2

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Ijumaa, 15 Februari 2013 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

### FASIHI KWA UJUMLA

1. "Fasihi simulizi huchomoza katika jamii ambayo inaandamwa na mabadiliko ya namna mbalimbali". Thibitisha dai hili kwa kutumia hoja tano ukionesha mabadiliko ya uhifadhi wa fasihi simulizi.

2. Ushairi na tamthiliya ni tanzu za fasihi andishi zenye kufanana na kutofautiana. Tumia hoja tano kuthibitisha tofauti na tatu kuonesha mfanano.

## SEHEMU B (alama 20)

### USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | **Haji Gora** |
| **Mapenzi Bora** | - | **Shaaban Robert** |
| **Chungu Tamu** | - | **Theobald A. Mvungi** |
| **Fungate ya Uhuru** | - | **Mohamed S. Khatibu** |

3. "Kazi ya fasihi hupata uhai wake kutokana na hali halisi ya maisha katika jamii." Kubali kauli hii kwa kutumia hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili ulizozisoma.

4. "Waandishi wa mashairi wamejaribu kujenga uhusiano na maadili mema miongoni mwa wanajamii kupitia tungo zao." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

## SEHEMU C (alama 20)

### RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| **Usiku Utakapokwisha** | - | **Mbunda Msokile** |
| **Kufikirika** | - | **Shaaban Robert** |
| **Mfadhili** | - | **Hussein Tuwa** |
| **Vuta N'kuvute** | - | **Shafi Adam Shafi** |

5. "Maisha ya wasanii ni kilio cha kudai haki za wanyonge." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.

6. "Kazi nzuri ya fasihi inajidhihirisha kupitia uwiano mzuri wa fani na maudhui." Jadili dai hili kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu zinazoonesha jinsi fani ilivyobeba maudhui kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 20)

## TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - | **Ebrahim Hussein** |
| **Morani** | - | **Emmanuel Mbogo** |
| **Kivuli Kinaishi** | - | **Said Mohamed** |
| **Nguzo Mama** | - | **Penina Muhando** |

7. "Fikra zenye kuleta mabadiliko ya haraka huhitajika katika kuondoa utendaji mbovu." Jadili kauli hii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili ulizosoma.

8. Ichambue dhana ya mapenzi halisi kama inavyojidhihirisha katika tamthiliya mbili ulizosoma, huku ukitoa hoja nne kwa kila tamthiliya.

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

9. Soma utenzi huu kisha jibu maswali yanayofuata:

Ulimwengu kama huu,
Wa chini kuwa wa juu,
Wadogo kuwa wakuu,
Na mchache wa nafuu,
Kitu kikubwa ni suluhu.

Ulimwengu kama huu,
Wa madhara ya miguu,
Vichwa vikawa mafuu,
Na siku si sikukuu,
Roho zataka suluhu.

Ulimwengu kama huu,
Wa magomvi na **malau**
Na njaa kubwa na kiu,
Kwa wana na wajukuu,
Watu wataka suluhu.

Ulimwengu kama huu,
Wa tambarare na **nguu**,
Ghasi na mau mau,
Wenye sheria na mbiu,
Wote twapenda suluhu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Ulimwengu kama huu,
Wa heshima na dharau,
**Weledi** na **mahahau**,
Mataradhio makuu,
Ya kila mtu suluhu.

Ulimwengu kama huu,
Wa ugali si pilau,
**Karela** si zambarau,
Na wekundu si bluu,
Haja kubwa ni suluhu.

Ulimwengu kama huu,
Wa tumbaku na kakau,
Na wa chai **tambuu**,
Bei zinapanda juu,
Jambo bora ni suluhu.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha utenzi huu.

(b) Eleza maana ya kila neno lililokolezwa wino kwenye utenzi huu.

(c) Unafikiri mwandishi wa utenzi huu anakusudia kuwapa ujumbe upi wasomaji wake? Eleza kwa kutoa hoja mbili.

(d) Utenzi huu ni wa aina gani? Toa sababu mbili kufafanua jibu lako.

(e) Eleza msisitizo wa mwandishi uliotokana na takriri zilizotumika katika utenzi huu. Chagua takriri tatu na uzifafanue.

10. Soma habari ifuatayo, kisha eleza mbinu za kisanaa zilizotumika na jinsi zilivyotumiwa.

Uhasama kati ya Boaz na Jeta sasa ulidhihirika. Baada ya tukio la fumanizi, Nimon hakutaka kuongea na Boaz tena. Badala yake, kila alipokuwa bwaloni, aliongea na Jeta. Tena wakati huo kuna kila dalili kuwa walihusiana kimapenzi.

Boaz alijigonga kwa Nimon na kumtaka radhi. Lakini sijui maombi yake yangesikilizwa vipi wakati hakuweza hata kumsogelea Nimon mwenyewe. Hata akiwa karibu nae alishona mdomo kwa uzi wa shaba na kuchomelea kwa risasi.

"Nimon, nisamehe, nimekosa," Boaz aliomba radhi. "Nilifanya makosa kukuficha habari za Anita. Hayo yamekwisha, tutazame mengine." Maneno hayo yalizidi kumchengua Nimon. Badala yake, mrembo huyo alimfuata Jeta huku akimwita hadharani, "Mpenzi Jeta, una mpango gani wa Jumapili hii?"

Jeta alikuwa mwenye soni sana. Hakujibu mbele ya watu akijua wazi kuwa Boaz alikuwa karibu. Lakini kimya chake kilimridhisha Nimon zaidi na kumchukiza Boaz. Boaz aliona kuwa ni majivuno. Nimon alimsogelea Jeta na kumgusa begani na kuacha mkono wake utulie pale huku akimwangalia Jeta machoni kwa uchokozi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Ama kweli mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu. Haya yalimuumiza Boaz, akawa mnyonge, aliyawaza mengi. Alitamani hata kukimbia kambi kama mwasi, lakini hilo lisingekuwa na faida kwake kwani ulikuwa umebaki mwezi mmoja tu wamalize awamu ya kwanza ya miezi sita, halafu watawanywe kwenye makambi mengine. Ndipo alipoamua kumwandikia barua Nimon. Sehemu ya barua yake nzito ilisomeka hivi:

*MPENZI Nimon,*
*Salamu. Waama baada ya salamu, usishangae kuwa nakuandikia barua badala ya kukuona wakati tupo wote hapa kambini. Nimejitahidi kila namna nikueleze binafsi dukuduku langu la moyoni; lakini kila mara hunipiga chenga ya moyo.*

*Mpenzi Nimon, binadamu hukosea na hili linaeleweka. Hata binadamu waliogombana hupatanishwa. Isitoshe, wewe au mimi kwa hali yoyote ile tunategemea msamaha toka kwa Mungu.*

*Tafadhali sana tusahau yaliyopita, kama ungekuwa rafiki tu tungeachia ngazi. Suala hapa ni uchumba, maana lengo langu hasa ni kuoana nawe.*

*Pia, ni vipi upoteze wakati na huyo hohehahe, Jeta? Au tuseme hiyo ndiyo namna ya kunikomoa? Jambo hili halivumiliki kwangu, maana linanitia kichefuchefu, uchungu na aibu pia.*

*Mpenzi, nimeona ufikiri tena na utazame nyuma tulikotoka wewe nami.*

*Wasalamu,*
*Ndimi, Boaz.*

Sehemu hiyo ya barua ndiyo hasa iliyomgusa Nimon. Mtoto wa watu hakawii kushikwa na hisia za mtu. Jumapili iliyofuata Nimon na Jeta walikutana mafichoni kama kawaida yao. Hapo ndipo Nimon alipomsimulia Jeta juu ya Anita.

Jeta hasa akajiona aliyebahatika kupendwa, hakuwa na wivu. Zaidi alimshauri Nimon.
"Mpenzi, Jeta alisema. "Kama Boaz ana nia njema nawe yafaa uheshimu hilo. Lakini ujue kama tutaendelea na hila hizi hasa kumwonyesha unyama, huenda akawa na chuki kali dhidi yangu."

"Potelea mbali." Nimon alisema." Ujue mapenzi huwa kama mmea. Ni mbegu tu inayokuja kuchipua. Kisha mmea unakua na kuzaa matunda. Siku moja ukinyauka na kufa siyo ajabu!"
Ingawa Jeta hakuridhika na majibu hayo hakuacha kujiuliza, "Lakini kuchagua kupo, bado sijachelewa. Huyu Nimon ana sababu zake za kunichagua hohehahe kama mimi. Kwanini sasa nisitamke ukweli?"

Nimon, ingawa alikuwa na uhakika na penzi la Jeta aligundua kuwa kulikuwa na mabadiliko.
"Mbona unaonekana kuwa mbali na hapa?" Nimon aliuliza. "Kuna jambo gani unaloliwaza?"
"Sikiliza ewe mwana kung'ara!" Jeta alisema. "Tumezoeana kiasi cha kutosha, kwanini tusiweke ahadi ya kuoana. Hakika ukiwa mchumba wangu nitafurahi sana."

"Hata mimi," Nimon alisema. "Najua tutapata kozi baada ya hapa na mwisho ajira. Tukiajiriwa tunaweza kuishi pamoja."



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org